TANGAZO LA SERIKALI NA. 414 la tarehe 24/05/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imegengenezwa chini ya kifungu cha 16 (1))*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA STENDI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME YA MWAKA 2024

Jina

1.- Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Stendi ya Halmashauri ya Wilaya ya Same za Mwaka 2024.

Matumizi

2.- Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya wilaya ya Same.

Tafsiri

3.- Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya wilaya ya Same;

"mabasi" maana yake magari yote yanayosafirisha au

kubeba abiria ila hayahusishi taksi;

"mabasi makubwa" maana yake ni mabasi yote yenye uwezo wa kubeba abiria 36 au zaidi;

"mabasi ya kati" maana yake ni mabasi yanayobeba abiria 21 hadi 35;

"mabasi madogo" maana yake ni mabasi yote yenye uwezo wa kubeba abiria wasiozidi 20;

"mmiliki" maana yake ni mtu mwenye gari, dereva, kondakta au mtu mwingine yeyote aliyeidhinishwa na mwenye gari kuwa na mamlaka ya juu ya gari wakati inaingia stendi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya ya Same au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hiii;

Sura ya 290 "Sheria" maana yake ni sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa;

"stendi" maana yake ni eneo maalum lililotengwa au kujengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, shirika, taasisi au kampuni ambayo limeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi yoyote chini ya Sheria Ndogo hii kwa niaba ya Halmashauri;

Ushuru wa stendi

4.- (1) Halmashauri itatoza ushuru wa stendi kwa vyombo vyote vya usafiri kwa mujibu wa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), ushuru wa kuingiza abiria stendi utalipwa na mmiliki wa gari, dereva, kondakta au mtu mwingine yeyote atakayepewa madaraka na mwenye gari kufanya hivyo kwa ushuru huo kukabidhiwa kwa wakala.

(3) Vyombo vya usafiri vinavyomilikiliwa na Serikali, Wanadiplomasia, majeshi na magari ya kubeba wagonjwa havitatozwa ushuru wa stendi.

Uanzishaji wa stendi

5.- (1) Halmashauri itaanzisha stendi itakayotumika kupakia au kushusha abiria na mizigo.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kuanzisha stendi ndogo katika maeneo ya vijiji kadri Halmashauri itakavyoona inafaa.

Wajibu wa kufanya usafi eneo la stendi

6.- (1) Kila dereva, dbiria au mtu yeyote anayetumia stendi atakuwa na wajibu wa kutunza usafi wa maeneo ya stendi.

(2) Mtu yeyote hataruhusiwa kutupa takataka za

aina yoyote katika maeneo ya stendi yasiyoruhusiwa.

Kushusha na kupakia abiria

7.- (1) Mabasi yote yatokayo au kuelekea Dar es Salaam, Moshi, Mwanga Korogwe, Hedaru, Makanya, Kisiwani, Ndungu, Myamba, Mwembe, Chome, Vudee na Ruvu yatalazimika kuingia Stendi Kuu.

(2) Mtu yeyote hataruhusiwa kusimamisha basi kwa madhumuni ya kushusha au kupakia abiria sehemu isiyoidhinishwa kuwa ni stendi.

(3) Kila mmiliki ambaye gari lake litakuwa limekamatwa na kuhifadhiwa karakana kutokana na kukiuka Sheria Ndogo hii atalipa gharama ya kuhifadhi gari lake.

Mamlaka ya afisa mwidhiniwa

8.-(1) Afisa mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kukamata na kuondoa chombo cha usafiri ambacho kitapakia au kushusha abiria nje ya eneo la stendi.

(2) Chombo cha usafiri kilichokamatwa kwa mujibu wa masharti ya aya ndogo ya (1), kitaondolewa na kuhifadhiwa kwenye yadi ya Halmashauri au sehemu yoyote kama itakavyoamriwa na Mkurugenzi.

(3) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuuza chombo kilichokamatwa baada ya kupata idhini ya Mahakama iwapo mmiliki wa chombo hicho atashindwa

kulipa gharama za uangalizi pamoja na gharama za kukamata chombo hicho ndani ya siku 14 tangu tarehe ya kukamatwa.

(4) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa kwenye aya ndogo ya (3), Halmashauri kabla ya kuuza chombo kilichokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya maandishi kwa umma juu ya kusudio la kuuza chombo hicho.

(5) Halmashauri haitawajibika na hasara yoyote na kwa namna yoyote ile itakayotokea wakati wa kukamata au kushikilia mali iliyokamatwa isipokuwa pale itakapobainika kuwa Halmashauri ilitumia mamlaka yake kinyume na Sheria.

Uteuzi wa wakala

9.- (1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kukusanya ada au ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa aya ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea ada au ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii;

(b) kukusanya ada au ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote

kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Uvaaji wa vitambulisho

10.- Wafanyakazi wote wa mabasi wanaojihusisha na uuzaji wa tiketi sehemu za Stendi kuu watalazimika kuvaa sare na vitambulisho vitakavyokuwa vinawatambulisha kuwa wao ni mawakala.

Makosa

11.- Kila mmiliki wa gari katika eneo la Halmashauri atakuwa ametenda kosa endapo-

(a) atagoma kuingiza gari lake ndani ya stendi;

(b) ataosha au kutengeneza gari ndani ya stendi;

(c) atatoa lugha ya matusi;

(d) atasababisha au kuleta usumbufu wowote kwa abiria;

(e) atafanya uharibifu wowote ndani ya stendi;

(f) atakayesimama na kupakia au kushusha abiria nje ya eneo la stendi;

(g) atakayekataa kupitisha gari lake Stendi kuu pamoja na stendi yeyote itakayoidhinishwa na Halmashauri;

(h) atakwepa au kushindwa kulipa ushuru uliopangwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Adhabu

12.Mtu yeyote anayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hii anatenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyotea.

Kufifilisha kosa

Sura ya 290

13.- Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizo kwa kuzingatia Sheria, iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi na kulipa ushuru anaodaiwa.

**JEDWALI LA KWANZA**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4 (1)*

**VIWANGO VYA USHURU WA STENDI**

| NAMBA | AINA YA TOZO | KIASI CHA TOZO (SHILINGI) |
|---|---|---|
| 1. | Mabasi madogo | 1,000/= kwa safari |
| 2. | Mabasi ya kati | 1,500/= kwa safari |
| 3. | Mabasi makubwa | 2,000/= kwa safari |
| 4 | Magari binafsi | 1,000/=kwa siku |

| | | |
|---|---|---|
| 5 | Texi | 1,000/=kwa siku |
| 6 | Bajaji | 300/=kwa siku |
| 7 | Pikipiki | 200/=kwa siku |
| 8 | Ada ya kutunza gari lililokamatwa au kuzuiliwa | 10,000/= kwa siku |
| 9 | Ada ya maegesho | 2,000/= Malori kwa siku<br><br>5,000/=Mitambo ya ujenzi kwa siku |

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 13)*

**FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA**

Mimi.............................................................nakiri **KWA HIARI YANGU MWENYEWE** mbele ya ................................................................ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, kwamba mnamo tarehe..........ya mwezi.......................Mwaka...........................nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Aya ya ...............ya Sheria Ndogo ya (Ushuru wa Stendi) ya Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka, 2024.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halamashauri ya Wilaya ya Same, niko tayari kulipa kiasi cha ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

**NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU NA KADRI YA UFAHAMU WANGU.**

Leo tarehe.....................ya Mwezi.........................Mwaka......................................

Jina.................................................... Saini.............................................................

Mbele ya:

Jina:............................................................

Wadhifa:.....................................................

Saini............................................................

Tarehe.........................................................

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Same imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 05 Mwezi Mei Mwaka 2023, Mbele ya;

ANASTAZIA TUTUBA
*Mkurugenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Same*

YUSTO MAPANDE (DIWANI)
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Same*

NAKUBALI,

**L.S**

Dodoma
25 Machi 2024.

MOHAMED OMARY MCHENGERWA(MB)
*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais*
*Tawala za Mikoa Na Serikali*